

HEROIN

Heroin ni aina ya dawa ya kulevya inayotokana na mmea unaojulikana kama afyuni (*Opium poppy*).

Kilimo cha mmea wa afyuni hufanyika kwa kiwango kikubwa sana katika nchi ya Afghanistani. Vilevile mmea huu hulimwa kwa kiwango kidogo katika nchi ya Misri.

Dawa hii hupumbaza mfumo wa fahamu na kumsababishia mtu kupata usingizi, kupungua kwa mawazo na maumivu mwilini.

Heroin huingizwa hapa inchini kwa kutumia njia mbalimbali kama vile anga na maji ikitokea inchi za Mashariki ya mbali



Muonekano wa heroin

MAJINA MENGINE YA HEROIN

- Unga
- Brown sugar
- Ngoma
- Ubuyu
- Mondo
- Dume
- Farasi
- Ponda



Heroin iliyofungwa maarufu kama "pipi"

NINI MADHARA YA HEROIN

- Kuharibika kwa mfumo wa fahamu,
- Kupata njozi,
- Kupata magonjwa ya moyo, ini, kifua na mapafu,
- Kushuka kwa mapigo ya moyo na shinikizo la damu,

- Kupungua kwa hisia na uwezo wa kuhisi maumivu,
- Kuhisi kupumzika,
- Kwa watumiaji wa heroin kwa njia ya kujidunga huweza kuambukizwa virusi vya ukimwi kwa kuwa watumiaji hushirikiana sindano,
- Kukosa umakini, kuzubaa, na kupungua uwezo wa kufanya kazi,
- Kupata kizunguzungu, kichefuchefu, kutapika na kufunga choo,
- Dozi kubwa husababisha kifo,
- Ikichanganyika na pombe mwilini, madhara huwa makubwa zaidi ikiwa ni pamoja na kifo,
- Mabadiliko ya hedhi kwa wanawake,
- Hujenga hali ya uteja kwa haraka sana kuliko dawa zingine za kulevya,

MADHARA KWA WAJAWAZITO

- Upungufu wa damu,
- Mimba kuharibika,
- Kuzaa watoto njiti,
- Watoto kupata matatizo ya kiafya yakiwemo kuchelewa kukua kiakili na kimwili,
- Kujifungua watoto ambao mara nyingi hufa wakiwa na umri chini ya miaka mitano.

MADHARA YA KIJAMII

- Kuvunjika kwa ndoa,
- Kutoweka amani,
- Kuongezeka kwa fujo, vurugu, uhalifu n.k.

- Kuongezeka kwa matatizo baina ya mwajiri na mwajiriwa,
- Kuchangia ongezeko la umaskini,
- Ongezeko la mzigo kwa Vyombo vya Ulinzi na Usalama na Taifa kwa ujumla.

NAMNA YA KUJIEPUSHA NA UTUMIAJI WA DAWA ZA KULEVYA

- Jiepushe na makundi ya watumiaji wa dawa za kulevya,
- Shiriki kwenye michezo mbalimbali,
- Jifunze na zingatia stadi za maisha.

SHERIA INASEMAJE KUHUSU HEROIN

Kutumia, kuuza, kusafirisha, kuhifadhi au kujihusisha kwa namna yoyote ile na Heroin ni kosa la jinai. Adhabu kwa makosa hayo hufikia hadi kifungo cha maisha.

JUKUMU LA MAABARA YA MKEMIA MKUU WA SERIKALI

Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali unalo jukumu la kufanya uchunguzi wa kitaalamu ili kubaini, kutambua na kuthibitisha aina na madhara ya dawa za kulevya.

KWA USHAURI NA MSAADA:

Nenda kwenye kituo cha Ushauri Nasaha au Kituo cha Afya kilicho karibu nawe.

Kwa maelezo zaidi wasiliana na:
Mkemia Mkuu wa Serikali
Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali
 Luthuli/ Barack Obama Drive
 S.L.P. 164
Dar Es Salaam, Tanzania
 Simu: + 255 22 2113383/4
 Nukushi: +255 22 2113320
 Barua pepe: cgc@gcla.go.tz, gcla@gcla.go.tz

Meneja
Maabara ya Kanda ya Mashariki
 Luthuli/Barack Obama Drive
 S.L.P. 164
Dar Es Salaam, Tanzania
 Simu: + 255 22 2113383/4
 Nukushi: +255 22 2113320
 Barua pepe: gcla.east@gcla.go.tz

Meneja
Maabara ya Kanda ya Ziwa,
 Eneo la Hospitali ya Sekou Toure/Isamilo
 S.L.P. 502,
Mwanza, Tanzania.
 Simu: +255 28 2500279
 Barua pepe: gcla.lake@gcla.go.tz

Meneja
Maabara ya Kanda ya Kaskazini
 Kituo cha Afya Them
 S.L.P. 2095
Arusha, Tanzania.
 Simu: +255 27 2506394
 Nukushi: +255 27 2549026
 Barua pepe: gcla.north@gcla.go.tz

Meneja
Maabara ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini
 Eneo la Hospitali ya Mkoa wa Mbeya
 New Forest Area
 S.L.P. 2875
Mbeya, Tanzania.
 Simu: +255 25 2502311
 Nukushi: +25525 250 312
 Barua pepe: gcla.southern@gcla.go.tz

Meneja
Maabara ya Kanda ya Kusini
 Ushirika House
 Barabara ya TANU
 S.L.P. 1414
Mtwara, Tanzania.
 Simu: +255 23 233 4760
 Nukushi: +255 23 233 4761
 Barua pepe: gcla.south@gcla.go.tz

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII,
JINSIA, WAZEE NA WATOTO



WAKALA WA MAABARA YA MKEMIA MKUU WA SERIKALI

ISO 9001:2008
 ISO 17025:2005

IDARA YA SAYANSI JINAI NA HUDUMA ZA VINASABA

IFAHAMU HEROIN NA MADHARA YAKE



KITENGO CHA SAYANSI JINAI – KEMIA (FORENSIC CHEMISTRY)